

## Maswali

1. Ilikuwa siku gani muhimu yenye wanafunzi walikusanyika pamoja?
2. Nini ilifanyika?
3. Wanafunzi walifanya nini?
4. Wayahudi walifikiria nini waliposikia wanafunzi wakizungumza lugha nyingi tofauti?
5. Petro alisema waliweza kuzungumza lugha tofauti namna gani?
6. Petro alisema watu waovu walifanya nini?
7. Mbona Wayahudi walikuwa na hofu?
8. Waliambia Petro nini?
9. Petro aliwambia wafanye nini?
10. Nini itafanyika ikiwa wakibatizwa?
11. Watu wangapi walibatizwa?

## Majibu

1. Ilikuwa siku ya Pentekoste.
2. Kulikuwa na sauti kubwa ya upepo. Ndimi za moto zilitua kwa wanafunzi.
3. Wanafunzi waliweza kuzungumza lugha nyingi tofauti?
4. Wayahudi walifikiria kwamba wanafunzi wamelewa.
5. Petro aliwambia kwamba walizungumza lugha tofauti kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
6. Petro alisema kwamba watu waovu waliua Yesu Mwana wa Mungu.
7. Wayahudi walikuwa na hofu kwa sababu walikuwa wameua Mwana wa Mungu.
8. Waliuliza Petro, “Tufanya nini?”
9. Petro aliwambia watubu (kusikitika) na wabatizwe.
10. Wakibatizwa watasamehewa dhambi zao.
11. Karibu watu elfu tatu walibatizwa.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



# 46 Siku ya Pentekoste

## Marejeo

Matendo ya Mitume 2: 1 – 8 na 12 – 16 na 36 – 38

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yesu alipea wanafunzi nguvu sisizo za kawaida ili wahubiri habari ya Injili ya wokovu.

## Maneno maalum

- 46.1 Siku ya Pentekoste + wanafunzi + sauti kuu, upepo wa kasi + ndimi za moto
- 46.2 Roho Mtakatifu + lugha tofauti + Wayahudi + nchi nyingi + vipi? + lazima wamelewa
- 46.3 Petro + hawajalewa + Roho Mtakatifu + Yesu Mwana wa Mungu + watu waovu + ua Yesu + Wayahudi + ogopa + tutafanya nini
- 46.4 Petro + tubu + Batizwa + samehewa + wengi walibatizwa + elfu tatu + samahewa

**46.1** Yesu alikuwa ameenda Mbinguni kuishi na Mungu. Siku ya Pentekoste wanafunzi walikusanyika pamoja kwa nyumba moja. Ilikuwa siku ya hamsini tangu Yesu afufuliwe kutoka kwa wafu. Wanafunzi walipokuwa wamekaa wanazungumza juu ya Yesu, mara kukatokea sauti ya upepo kubwa na ya kasi. Huo upepo uliunguruma ukizunguka hiyo nyumba kwa sauti ya juu.



Wanafunzi waliangaliana. Wakiuliza, “Nini inafanyika?” Halafu wakaona juu ya kila mmoja wao kulikuwa na ndimi za moto.

**46.2** Roho Mtakatifu wa Mungu alikuwa amekuja kwa kila mwanafunzi. Walipoanza kuzungumza, walijikuta kwamba kila mmoja alikuwa ananena kwa lugha tofauti.

Inachukuwa muda mrefu kwa mtu kujifunza lugha ingine. Lakini hawa watu waliweza kuzungumza lugha zingine bila kujifunza. Huu ulikuwa muujiza.

Wayahudi wengi walikuwa wamekuja Yerusalemu kwa siku ya Pentekoste. Watu walikuwa wamekuja kutoka kwa nchi tofauti za ulimwengu. Waliwasikia wanafunzi kila mmoja akisema kwa lugha zao zenye wanasikia. Walishangaa na kuuliza, “Nini inafanyika? Hawa watu ni wavuvi kutoka Galilaya, mbona wanazungumza lugha nyingi tofauti?”

Hawakuelewa hata kidogo. “Hii ina maana gani?” Waliuliza. Wengine walisema, “Hawa wamelewa.” Petro aliwasikia wakisema hivyo.

**46.3** Petro alisema, “Hapana! Hawa watu hawajalewa. Nimapema sana kulewa. Haya ni yale nabii Yoeli alisema itafanyika, aliposema, Mungu atamwaga Roho wake kwa sisi.”

Wayahudi walisikiliza Petro akiwambia kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, ndiye Mfalme wao. Watu waovu walimuua lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu.

Watu walimwalia Petro. Wengi wao walikuwa ni baadhi ya waliomuona Yesu akiwa amesima mbele ya Pilato aliyekuwa liwali. Pilato alisema, “Tazama Mfalme wenu! Nimfanye nini?” Walikuwa wamepaza sauti wakisema, “Asulibiwe! Asulibiwe!”

Wayahudi waliangalia Petro na hofu kuu. Walikuwa wamesulibisha Mfalme wao. Yesu hakukuwa tu Mfalme wao, lakini alikuwa Mwana wa Mungu pia. Walimuuliza Petro, “Tufanye nini basi?”

**46.4** Petro aliangalia nyuso za Wayahudi zilizokuwa na uoga. Akawambia, “Lazima kila mmoja wenu atubu na abatizwe katika jina la Yesu kwa ondoleo la dhambi.”

Kwa hivyo wengi wao walibatizwa na Petro na mitume wengine. Walikuwa karibu watu elfu tatu. Baada ya kubatizwa, walijua kwamba Mungu alikuwa amewasamehe dhambi zao. Alikuwa amewasamehe kwa ajili ya Yesu.

Tukikua wakubwa halafu tujifunze juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu waajabu, tunaweza kubatizwa. Halafu Mungu atatusamehe, atubariki na atatupa mahali kwa Ufalme Wake.